



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA  
MAMLAKA YA MAENDELEO YA BIASHARA  
TANZANIA (TANTRADE)



TAARIFA KWA UMMA

KUANDAA MAONESHU, MAKONGAMANO NA MISAFARA YA KIBIASHARA  
NDANI NA NJE YA TANZANIA

Dar es Salaam - 24 Oktoba, 2024

Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) inapenda kutoa taarifa kwa Umma juu ya wimbi la kuandaa , Maonesho (Trade Fairs and Exhibitions) Makongamano, Misafara ya Kibiashara (Trade Missions) pamoja na shughuli nyingine za Ukuzaji Biashara (Trade Promotional Events) ndani na nje ya Nchi yasiyokua na kibali rasmi na nje ya ratiba ya Kitaifa.

Tunawajulisha Umma, Wizara, Mikoa, Wilaya, na Halmashauri zote pamoja na Sekta binafsi kuwa waandaaji wa shughuli hizo wanapaswa kufuata taratibu zilizowekwa kwa kupata kibali cha Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade).

Kifungu cha 5(1) (b) cha Sheria ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade), Na. 4 ya mwaka 2009 pamoja na marekebisho yake, kimeipa TanTrade mamlaka ya kuunganisha na kudhibiti Soko la Ndani (Integrate and Regulate Domestic Market). Uratibu wa shughuli za Ukuzaji Biashara ni sehemu ya utekelezaji wa matakwa hayo. Kadhalika, Kifungu cha 5(1). (p) cha Sheria hiyo pamoja na Aya ya 3(1)(k) ya Kanuni za Sheria ya TanTrade za mwaka 2010, vinaipa TanTrade mamlaka ya kumuhusu/ kutoa kibali kwa mtu yeyote, Taasisi au Shirika lolote kuandaa Maonesho ya ndani (local) na ya Kimataifa (International).

Ikumbukwe kuwa ni kosa kisheria kufanya Maonesho, Makongamano, Misafara ya kibiashara, pamoja na shughuli nyingine za ukuzaji wa biashara bila kuwa na kibali kutoka TanTrade.

Kwa maelezo zaidi tafadhali wasiliana nasi kupitia simu namba **0733 002 014** au tembelea tovuti yetu [www.tantrade.go.tz](http://www.tantrade.go.tz) au fika katika Ofisi zetu zilizopo katika Uwanja wa Maonesho wa Mwl. JK Nyerere, Barabara ya Kilwa, Dar es Salaam au Jengo la Kilimo V, Barabara ya VETA nyuma ya CBE, Dodoma na Zanzibar, Kijangwani, Jengo la Posta.

Imetolewa na,

Latifa M. Khamis  
MKURUGENZI MKUU